(20) Idadi ya watu itaongezeka lakini wakiikhtilafiana baina yao
(21) Ahadi na mikataba itakuwa ikivunjwa kila hapa na pale
(22) Wanawake watakuwa wakishirikiana pamoja na wanaumeError: Reference source not found wao kwa uroho wa mali

(23) Sauti za Wakomunisti na wapingamizi wa Dini zitakuwa zina nguvu sana.
(24). Nao watakuwa wakisikilizwa na kila mtu
(25). Viongozi wa Jumuiya watakuwa ndio watu waovu kabisa
(26) Watu waendeshao biashara za Mabenki watakuwa wabadhirifu na wadhulumaji
(27). Ala za muziki zitakuwa zikipatikana kila mahala na kupindukia idadi.
(28). wanawake watakuwa wakipanda mafarasi na wakiendesha magari.
(29). Kuiga, hali ya mtu mwingine itaonekana ni kama desturi ya kawaida yaani mwanamme atapenda awe kama mwanamke (ajifanye mwanamke)na mwanamke atapenda ajifanye kama mwanamme6.
(30). Utatolewa ushahidi katika mambo ya mahakama ingawaje mtoa ushahidi mwenyewe atakuwa haelewi kitu chochote kuhusu kesi inayoendelea lakini atatoa ushahidi wa kiuongo katika kesi yoyote ile itakayokuwa ikiendelea
(31). Mbwamwitu watakuwa wengi , katika makundi ya kondoo.
(32) Unafiki utakuwa ndio mambo ya kujivunia .
(33) Nyoyo za watu zitakuwa zikinuka kuliko hata maiti na mbaya kabisa kuliko kitu chochote kile
(34) Na mahali pa kuishi pema kabisa wakati huo itakuwa ni Jerusalem. Utafika wakati huo mtu atatamani laiti angelikuwa mkazi wa Jerusalem.
Asbagh ibn Nabata alisimama na kusema "Ewe Bwana, naomba utwambie DajjalError: Reference source not found atakuwa ni mtu wa aina gani?"
Imam Ali a.s. alimjibu "Yeye atakuwa ni Sayyed . Laana iwe kwa mtu atakaye mkubalia DajjalError: Reference source not found na atakuwa mtu mwenye bahati yule ambaye atakuwa amemkana Dajjal.
(35). Yeye atatokea karibu na Kijiji kinachojulikana kama Isbahan kutokea eneo la Judea, kutakuwa na toto la jicho katika jicho la kulia . Jicho lake la kushoto litakuwa juu ya paji lake la uso na litakuwa liking'ara kama nyotaError: Reference source not found ya alfajiri, na hapo kutakuwa kipande cha nyama kilichojaa kwa damuError: Reference source not found. Baina ya macho yake mawili kutakuwa na herufi zilizoandikwa katika Kiarabu *Kafir* yeye atapita katika mabahari makubwa makubwa.
(36). Jua litakuwa pamoja naye.
(37). Wingu la moshi litakuwa mbele yake na mlima mweupe utakuwa nyuma yake.
(38). Watu waliofikwa na majanga ya njaa watafikiria hiyo milima kama ni chakula,
(39) Na punda wake mwekundu atakuwa akitembea mamaili na miguu yake itakuwa ikirefuka na kuwa mifupi kufuatana na ardhi ilivyotambaa.
(40) Maji yoyote atakayokuwa akiyapitia yeye DajjalError: Reference source not found yatakauka hadi siku ya QayamaError: Reference source not found,(41). baadaye atapiga sauti kwa nguvu kwamba kila kiumbe kitamsikia, atasema"Enyi marafiki! Mimi ndiye yule mliyekuwa mkinisubiri, mimi ndiye niliyewaumba, na niliyewafanya nyie mkawa wazuri. Na mimi ndiye mpaji wenu mkubwa sana. "
(42). Huyu mwehu wa jicho moja atakuwa mwongo mkubwa sana.
(43) Ole wenu, wafuasi wake wengi watakuwa ni wanaharamu na wale waliozaliwa kwa zinaaError: Reference source not found,
(44) wao watakuwa wakijivika vitambaa vya silki,
(45) huyo DajjalError: Reference source not found atauawa mahala panapoitwa Aqba huko SyriaError:

Reference source not found, atauawa siku ya Ijumaa mchana,
(46) Mtume Issa a.s. atasali nyuma ya Imam MahdiError: Reference source not found a.s.
(47) na baadaye jambo la ajabu kabisa litatokezea.

Yajuj na Majuj

Allah swt anasema katika Quran,**Sura 18 : 92 – 99.**

"*Kisha akaifuata njia.*
Hata alipofika katikati ya milima miwili, alikuta nyuma yake watu ambao waliweza kwa shida kufahamu neno (*wanaloambiwa*)*.*
Wakasema: "Ewe Dhulqarnain! Hakika Yajuj na Majuj wanafanya uharibifu katika ardhi. Basi je, tukupe ujira ili utie baina yetu na baina yao kizuizi?"
Akasema: "Yale ambayo Mola wangu amenimakinishia ni bora (*kuliko ujira wenu. Nitakufanyieni bure*)*;Lakini nIssaidieni kwa nguvu zenu. Nitaweka baina yenu na baina yao kizuizi chenye imara."*
Nileteeni vipande vya chuma. "Hata alipoijaza nafasi iliyo katikati ya milima miwili,alisema: "Pulizeni" mpaka alipokifanya (*kile chuma*) *kuwa moto, alisema "Nileteeni shaba iliyoyayuka niimwage juu yake. "*
Hivyo (*Yajuj na Majuj*) *hawakuweza kuukwea wala hawakuweza kuutoboa.*
Akasema: "Hili ni rehema itokayo kwa Mola wangu. Na itakapofika ahadi ya Mola wangu ya kufika QayamaError: Reference source not found)*,atauvunjavunja. Na ahadi ya Mola wangu ni kweli tu. "*

Yajuj na *Majuj* walikuwa ni viumbe vyenye miguu minne na wakifanana na wanaadamu kisura na wao walikuwa ni wafupi mno mbele ya watu wa zama hizo. Na watoto wao walikuwa wakizaliwa kama watoto wa wanaadamu na walikuwa hawakui zaidi ya shubiri tano na sura zao zilikuwa aina moja na walikuwa wazururaji. Kwa kuwa ngozi zao zilikuwa ngumu kama zile za ngamia, hivyo hawakuathirika kwa baridi wala joto. Walikuwa na makucha makubwa na meno makali na masikio yao yalikuwa marefu kiasi kwamba walikuwa wakitandika moja na kujifunika kwa la pili. Walikuwa wakiingiliana kama wanyama na chakula chao kikubwa kilikuwa ni samaki kwa sababu kulikuwa kukinyesha mvua za samaki, na kama kulikuwa na kasoro ya samaki basi walikuwa wakishambulia miji na kuchafua na kuvuruga kila kitu kiasi kwamba watu walipokuwa wakizisikia sauti zao, walikuwa wakikimbia na kuacha makazi yao kwa sababu ilikuwa ni vigumu mno kuwakabili kwani walipokuwa wakiingia mijini basi miji yote ilikuwa ikijaa wao tu. Idadi yao ilikuwa kubwa mno kiasi kwamba hakuna mtu mwingine ajuaye isipokuwa Allah swt. Wao walikuwa hawafi hadi wamezaa watoto zaidi ya elfu moja.

Katika vitabu tunapata habari zaidi kuwa Yajuj na Majuj ni makabila mawili yaliyokuwa makubwa kutokana na kizazi cha *Yafus*, mwana wa Mtume Nuh a.s. Na katika Agano la Kale, Majuj anaelezwa kuwa ni Chifu wa Mashech na Tunal. Kwa sasa Moscow ndio mto unaosimama mji huo, uitwao Moscow, mji mkuu wa Urusi; Tabul ni mto huko Urusi ambapo kuna mji Tobolsk.

Katika eneo la Ulaya ya Kusini na Urusi ya Kiasia, baina ya Wacarpathiani na Don, kulikaliwa katika enzi za zamani na kabila katili kabisa ambao waliiteka Asia ya Magharibi kuanzia karne ya 7 Kabla ya Kristo

hadi mwanzoni mwa kipindi cha Kikristo, wakati mashambulizi yao yalipokwisha kwa sababu ya Bwana Dhulqarnain alipoujenga huo ukuta.

Vile vile inasemekana kuwa neno *Mongol* ni mvurugano wa neno la Kichina *Mongog* au *Manchog* Iwapo utafiti huu utakuwa wa kweli, hivyo. Hivyo itamaanisha kuwa eneo la Yajuj na Majuj inaanzia Mto wa Moscow hadi Turkistan ya Kichina na Mangolia.

Maelezo ya 'kuta' katika Quran Tukufu yanaonyesha kuwa lazima iwe imejengwa pale penye njia ili kuzuia makabila hayo ya wachochezi na wakatili kuwashambulia majirani wao waliokuwa mafundi stadi katika kazi za kufua vyuma na walikuwa matajiri.

Sheikh Abul-Kalam Azad, katika moja ya makala yake (katika *Jannatul-Ma'arif*) anaelezea kuwa kuta hizo zimeendelea hadi Uturuki.

Ayatullah Agha Haji Mirza MahdiError: Reference source not found Puya Yazdi (katika hashia ya Tafsiri ya Quran iliyofanywa na S. V. Mir Ahmad Ali) anawanakili wengine wakisema kuwa kuta hizo zipo baina ya milima ya Armenia na Azerbaijan.

Hata hivyo kuna tofauti ya maoni kuhusu utambulisho wa Dhulqarnain. Abdullah Yusuf Ali anadhani kuwa jina hilo linaelezea kuwa ni Alexandar Mkuu wa Misri.

Wengineo, kama Agha Puya, wanafikiri kuwa huyo anatambulishwa kama ni Mfalme wa Kiajemi aliyekuwa akiitwa Darius.

Kwetu sisi hatumaanishi kuingia katika mazungumzo mengi kuhusu mjadala huu lakini inatubidi liwe jambo lililowazi mbele yetu kuwa kwa mujibu wa Quran Tukufu, Dhulqarnain alikuwa ni *mcha Mungu* hivyo kamwe haiwezekani kumtambulisha Dhulqarnain kama *kafiri* au *mpagani*.

Kwa mujibu wa Quran Tukufu, itakapokaribia Siku ya *QayamaError: Reference source not found*, kabila hizi zitafanikiwa kuvunja kuta, yaani zitaenea zaidi kuliko mipaka yao ya awali. Upanuzi huo unaweza kuwa kimantiki; ambapo inaweza kumaanisha kuwa itikadi zao (ukomunisti na ukafiri) zinaweza kuenezwa nje ya mipaka ya nchi zao. Au itakuwa aina ya kikoloni yaani kukalia maeneo ya mashariki ya Ulaya, Asia ya Kusini na maeneo mengineyo. Au inaweza kumaanisha yote.

Imeandikwa katika *Tafsir Majma-ul-Bayan* kuwa baada ya kuteka maeneo ya ardhi watajararibu kuiteka mbingu. "Hivyo watatupa mishale yao kuelekea angani, na itawarejea zikiwa na alama kama za damu. Hivyo watasema: 'Sisi tumekwishawateka wakazi wa dunia na tumewateka wakazi wa angani. "

Ni dhahiri kuwa *mishale* inamaanisha maroketi na vyombo vya angani. Maneno *itawarejea zikiwa na alama kama za damu* inamaanisha kuwa vyombo vya angani vitafikia malengo yao na kurejea duniani.

Kwa mujibu wa Tafsiri hiyo, "wakati watakapokuwa na takabari kubwa kwa sababu ya 'kushinda anga za juu', Allah swt atawaumba funza au minyoo ambayo itawaingia masikio yao, na kuwaua wote.

Inamaanisha kuwa hatima yao itakuwa kwa kuangamizwa kwa maafa makhsusi, au kwa magonjwa ya kuambukizwa yatakayotokana na vijidudu.

Dabbatul Ardh

Saasaan anaelezea zaidi: "Sisi tulimwuliza Imam Ali a.s. Je ni nini kitakachotokea baadaye?"
Ali a.s. alijibu: “Karibu na mlima *Saffa* na *Marwa,* Dabbatul Ardh atakuja. Yeye atakuwa na pete ya Mtume Suleiman na atakuwa na mkongojo wa Mtume Musa a.s. na yeye atakuwa akiiweka hiyo pete juu ya vipaji vya makafiri na loh ! kutatokezea dalili za kuonyesha kuwa huyu mtu ni kafiri, na ukafiri wake utaonekana usoni mwa mtu huyo aliyegusishwa pete ya Mtume Suleiman a.s. *Dabbatul ardh* pia atakuwa akiwaangalia waumini na ataweza kuwatambulisha kuwa wao ni waumini, yeye kwa amri ya Allah swt atakuwa akiangalia juu ya mbingu na ataweza kuona Mashariki na Magharibi papo hapo. Na tukio hili litatokezea baada ya jua kuchomoza kutoka Magharibi hapo ndipo milango ya *tawba* itakuwa imefungwa, muda wa kufanya *tawba* utakuwa umekwisha. Matendo na amali havitasaidia chochote. Ninawaombeni msiniulize baadaye kitakachotokea kwa sababu nimempa ahadi Mtume s.a.w.w kuwa sitaitoboa hii siri isipokuwa kwa yule atakayekuwa mrithi wangu. "
Mpashaji habari wa tukio hili Taran ibn Sabra alimwuliza Saasan ibn Suhan "Je nini maana hili jambo alililoliezea Imam Ali a.s."
Saasan alijibu: "Ewe ibn Sabra, Mtume Issa a.s. atasali nyuma ya Imam wa 12 (kumi na mbili) katika kizazi cha Imam Ali a.s. na ni mtu wa kizazi cha tisa (9) katika kizazi cha Husein ibn Ali a.s. Huyo atakuwa ni jua litakalo chomoza kutoka Magharibi, yeye ataitakasisha ardhi baina ya Rukn na Msikiti na ataeneza uadilifu duniani kote. Baada ya hapo hakutakuwapo na dhuluma ya aina yoyote. "

Kudhihiri Kwa Mtume Issa A.S. Kutoka Mbinguni

Ni imani ya Waisilamu wote kuwa Mtume Issa a.s. alikuwa hakusulubiwa wala hakuuliwa bali alichukuliwa na Allah swt katika mbingu za juu na yupo hai. Kwa wakati maalum uliowekwa na Allah swt, Mtume Issa a.s. atadhihiri duniani kutoka mbinguni hadi SyriaError: Reference source not found. Wakati huo Imam MahdiError: Reference source not found a.s. atakuwa humu humu duniani na Mtume Issa ataungana naye. Pamoja na Imam Mahdi a.s. wakati wa salaError: Reference source not found Imam Mahdi a.s. atakuwa akiongoza sala na Mtume Issa a.s. atakuwa akisali sala nyuma yake. Wao wote kwa pamoja watatangaza vita dhidi ya DajjalError: Reference source not found ambaye atauawa. Baada ya hapo WayahudiError: Reference source not found wote na Wakristo wote watakuwa Waislamu . *QuranError: Reference source not found* Tukufu inatupa habari kwa urefu na mapana kuhusu Mtume Issa a.s. vile vile tunapata habari nyingi sana katika Hadithi tukufu. Vile vile kulitokezea na mtu ambaye alidai kuwa Mtume Issa a.s. amekufa na yeye alikuwa ni masiha mtu huyo anajulikana kwa jina la Mirza Gulam Ahmad KadianiError: Reference source not foundError: Reference source not found, mimi sitapenda kuingilia maswala haya na kuyachambua kwani mambo haya yametobolewa khususani katika nchi ya Pakistani na serikali ya Pakistani imefichua siri za hawa watu na imetangaza kuwa wafuasi wa Kadiani si Waislamu na haya ndiyo yalikuwa maamuzi ya Mahakama yaliyosikiliza kesi zao. Iliyochukua

nafasi muhimu katika mahakama ya Pakistani .

Kuzagaa kwa Moto na Moshi Duniani

Allah swt anasema katika Quran, **Sura Ad –Dukhan 44:10–16**
Basi ingoje siku ambapo mbingu zitakapoleta moshi uliodhahiri.
Utakaowafunika watu; Hii ni adhabu iumizayo.
(*Wao watasema*) *'Mola wetu! Tuondolee adhabu hii hakika* (*sasa*) *mumin. '*
Nini faida ya kukumbuka kwao? Na alikwisha wajia Mtume abainishaye.
Wakampa kisogo na wakasema: 'Amefunzwa ni mwendawazimu.
Kwa yakini Sisi tutaiondoa adhabu kidogo, nyinyi mtarudia (*makosa yenu*).
(*Na itakuja*) *siku ambapo tutawateka* (*wote*) *kwa mteko mkubwa; Kwa hakika sisi ni wenye kulipiza.*

Kwa mujibu wa riwaya nyingi mno, Aya hizi zinabashiria moshi utakaokuwapo karibu na *QayamaError: Reference source not found. Moshi* huo utaingia katika masikio (na macho), na vichwa vya watu vitaonekana kama yamechomwa. Lakini haitawadhuru waumini; wao watahisi mwasho wa kawaida wa kama baridi. Na dunia nzima itakuwa mfano wa nyumba iliyoshika moto na ambayo haina madirisha wala sehemu za kutokezea moshi. Na sura hii itadumu kwa muda wa siku arobaini.

Dalili hii itakuwa ni ishara ya kuonywa; na kama inavyoonekana katika *Aya* wanaadamu watapewa muda wa kurejea katika imani na njia iliyo ya haki na wajirekebishe. Maneno '*Kwa hakika Sisi tutaiondoa adhabu kidogo'* inatudhihirishia kuwa moshi utaondolewa, lakini maneno yanayofuata *nyinyi mutarudia* (*makosa yenu*) inatuonyesha kuwa kuondolewa kwa adhabu hiyo tu, basi si watu wengi watakaotafakari juu ya suala hilo. Labda wengi watatafuta visingizio vya kijiografia au zinginezo kwa ajili ya kutokezea kwa adhabu hiyo, na watasahau ahadi zao walizompa Allah swt kuwa *Mola wetu !. . . hakika* (*sasa*) *muumin.*

Kwa hakika si vigumu kukubaliana na mambo yaliyoeelezwa hapo juu:
1. Umande na moshi unakuwapo hata leo hivyo Allah swt anao uwezo wa kuumba moshi utakaotanda duniani kote.
2. Allah swt anaweza kuwaepusha mumin kutokana na athari mbaya kabisa za moshi huo. Kwani hata leo tunaona kuwa si watu wote wanaoathirika na maafa yanapozuka katika maeneo fulani.
3. Na kuna idadi kubwa kabisa isiyohIssabika ya makafiri wanaotubu pale wanapopatwa na adhabu au matatizo,na husahau kwa urahisi ahadi zao kwaAllah swt (za kuwa mumin) za kuomba, mara baada ya kuondokea na matatizo yao.

Ubashiri huu umeelezwa katika vitabu vingi vya Hadith, kutakuwa na moshi mwingi sana katika anga zetu kwa sababu hiyo kutakuwapo kwa motoError: Reference source not found kila mahali.

Inawezekana ubashiri huu unadalilisha utumiaji wa aina nyingi za magesi ambayo yanalipuka yenye hatari na motoError: Reference source not found ndio utakuwa sababu ya gesi hizi, majaribio ya *nyukilia*

vile vile yanatoa gesi nyingi na miale ya *radio active* vile vile katika ubashiri mwingine imeelezwa kutakuwapo na moto unaotokea ndani mwa ardhi ya AdenError: Reference source not found, nimeelezea maswala haya katika kurasa zilizopita.

Kuangamizwa kwa Baghdad

Kuna mabashiri mengi katika kuelezea kuteketezwa kwa baadhi ya miji khususan kuteketezwa kwa mji wa BaghdadError: Reference source not found ndiyo imeelezwa kwa zaidi na wanazuoni wengi wanasema kuwa ubashiri huo ni wa kweli.
Imam Jaafer Sadiq a.s. alitoa hotuba ndefu sana kuhusiana na swala hilo. Imam Ali a.s. pia ameelezea kwa undani zaidi katika hotuba zake na hapa ninawachambulia machache kutoka hotuba hiyo: “Enyi watu kutabuniwa mji mpya utakaoitwa BaghdadError: Reference source not found (Labda alimaanisha Baghdad mpya) Mji huo utakithiri kwa madhambi na maasi kiasi kwamba adhabu za Allah swt zitakuwa zikilengwa sana huko. Balaa za kila aina zisizojulikana, magonjwa yakuangamiza, ukame, mafuriko ya mto Tigris na mvuaError: Reference source not found zisizo na mpangilio vile vile tufani za kila aina zitakuwa zikitokea kuuangamiza mji huo. Na kuangamizwa kwa mji huu kutatokea baada ya aina tatu za benderaError: Reference source not found kuchomoza katika mji huo. Bendera ya kwanza itakuwa rangi Njano, ya pili aina ya bendera itakuwa kutoka pande za magharibi, na ya tatu itatokezea sehemu za kuizunguka, na labda hii ndiyo dalili ya vita vya wenyewe kwa wenyewe.

Uasi Kuongozwa na Hasan Sayyid

Kijana huyu atakuwa mzuri na atakuwa ametokana na kizazi cha Imam Hasan a.s. na katika baadhi ya Hadith anapewa jina la Hasan, atatokezea kutoka kijiji cha Dailam (karibu na Kazvin) yeye hatajitangazia uongozi wowote wa kidini bali atakuwa akiwaita watu baada ya kuona hali ya jamii na jumuia imeharibika na kuvurugika, atawaita watu waache maovu na wajirekebishe. Watu wa Taliqan watakuwa ndio watu wa kwanza kuutikia wito wake. Watu watamzunguka na watajiunga kwa wingi katika harakati zake, ujumbe wake utaenea katika sehemu zinazozunguka za karibuni na kufikia hadi Multan kupitia Kirman na vile vile atafika BasraError: Reference source not found. Sehemu zote hizi zitakubaliana na mazungumzo na mambo yake. Baaada ya hapo ataelekea KufaError: Reference source not found na huko atapata habari kuwa Imam MahdiError: Reference source not found a.s. amedhihiri na Imam a.s. ameondoka kuelekea IraqError: Reference source not found kupitia *MakkahError: Reference source not found* na *MadinaError: Reference source not found*.
Wakazi wa KufaError: Reference source not found watakuwa wakiishi maisha yasiyo wafurahisha wao wenyewe. Huyu Hasan Sayyed ataonana na Imam MahdiError: Reference source not found a.s. kutaka kujua miujiza na uthibitisho wa uhalali wake wa kuwa Imam Mahdi a.s. baada ya kuthibitishiwa atakula kiapo kwa Imam Mahdi a.s. pamoja na jeshi lake la utiifu.
Imam Jaafer Sadiq a.s. amesema: “Kwa jina la Allah swt, Hasan Sayyed atakuwa akimtambua vyema kabisa Imam MahdiError: Reference source not found a.s. lakini ili kuwahakikishia watu na kuwathibitishia na kuwatolea shaka watu kuwa huyu ndiye Imam Mahdi a.s. atamuomba Imam

amthibitishie kwa miujiza uhalali wake. Wanajeshi elfu nne wa Zaid kutoka YemenError: Reference source not found watakaokuwa katika jeshi la Hasan Sayyed wataaasi. Hapo Imam Mahdi a.s. atamshauri Hasan Sayyed awatulize hao vijana wa kabila la Zaid wajisalimishe. Mazungumzo hayo yataendelea kwa muda wa siku tatu, lakini wanajeshi wa Zaid hawatakubali, hatimaye wote watauawa.

(4). Ubashiri Wa Siku Za Mbeleni

Kwa hakika mabashiri yafuatayo yanahitaji kuzingatiwa mno, hapa chini ninawaleteeni machache na nitawapa maelezo kidogo juu yake:

(1). Uasi wa Shuayb ibn Saleh
Yeye atakuwa ni mtu mwema na ataanzisha uasi wake katika mji wa Samarqand. Mambo mengi ya muhimu yatatokea wakati wake. Hadithi nyingi zinaelezea kuwa ama yeye atakuwa ni kamanda katika jeshi la Hasan Sayyed au Imam MahdiError: Reference source not found a.s.

(2). Uasi wa Aus
Huyu atakuwa ni mtu mwema atakayewaita watu katika mawazo yake baada ya vita vikuu, huyu mtu atakuwa amesimamia mapinduzi kutoka Kuwait hadi Syria ambapo ndipo atakapouawa.

(3). Uasi wa Yamani
Kutatokezea kwa mtu asiyejulikana kutokea huko YemenError: Reference source not found ambapo ataleta maangamizi na ataleta fitina na ugomvi wa hali ya juu sana.

(4). Maghrebi kuilinda MisriError: Reference source not found
Katika lugha ya Kiarabu Algeria,Tunisia,Morocco na Libya, zinaitwa *Maghreb* kutatokezea mtu katika nchi hizi yaani Maghreb ambaye atakuja MisriError: Reference source not found na atahukumu nchi hizo zote ikiwemo SyriaError: Reference source not found.

(5). Kuuawa kwa Mohammad Hasan Zakiyya
Imam Ja'afer as- Sadiq a.s. amesema: "Siku kumi na tano tokea kudhihiri kwa MahdiError: Reference source not found a.s. mtu mtakatifu sana kwa jina la Muhammad ibn Hasan Zakiyya ambaye atakuwa ni mmoja wa wafuasi wakubwa wa Imam Mahdi a.s. atauawa karibu na *Al-Ka'aba* baina ya *Rukn* na *Maqam*.

(6). Kutokezea kwa Ikhtilafu

Kutatokezea ikhtilafu kubwa sana miongoni mwa Bani Abbas.

(7). Mtu Maarufu sana
Mtu maarufu sana mcha Mungu ajulikanaye kwa jina la nafsi Zakiyyah atauawa pamoja na Sayyid sabini nyuma ya Msikiti wa KufaError: Reference source not found. Ukatili na mauaji haya ya kikatili yatatendwa na jeshi la *SufianiError: Reference source not found*.

(8). Mji wa MakkahError: Reference source not found
Mtu mmoja kutoka Bani Hashim, mcha Mungu kabisa atauawa katika mji wa *MakkahError: Reference source not found*.

(9). Mahakama ya KufaError: Reference source not found
Chumba cha Mahakama ya KufaError: Reference source not found kitaharibiwa pamoja na ukuta wa Msikiti wa Kufa.

(10). Theluji ya kushangaza
Kutakuwepo na kuanguka kwa theluji ya kushangaza katika Roma kila kipande cha theluji kitakuwa kama yai.

(11). Nyota ya kustaajabisha sana
Kutachomoza kwa nyotaError: Reference source not found kutoka Mashariki, mwanga wake utakuwa sawa na wa mwezi. Mkia wake utakuwa ukipotea pole pole na hatimaye kupotea. Nyota hizi za kuanguka zimekuwa zikitokea daima lakini hakuna hata moja ambayo imeweza kuwa na nuru kama mwezi.

(12). MotoError: Reference source not found katika anga za juu
Katika anga za juu baina ya anga na ardhi kutatokezea motoError: Reference source not found utakaowaka siku tatu mfululizo au siku saba kwa hakika litakuwa jambo kubwa la kustaajabisha.

(13). Rangi nzito mbinguni.

Rangi nzito nyekundu iliyoiva itazagaa mbinguni.

(14). MotoError: Reference source not found Mashariki ya Kati.
Kutakuwa na mioto ikiwaka kila mahala khususan Mashariki ya Kati. MotoError: Reference source not found utakuwa wa kutisha sana kiasi kwamba watu wataanza kutubu madhambi yao.

(15). Waarabu watakuwa ni watu wasiokuwa na msimamo:
Hakuna hata mmoja atakayeweza kumsaidia mwenzake kwa moyo kwani kila mmoja atakuwa akitenda vile atakavyo kwa masilahi yake mwenyewe.

(16). Mfalme wa IranError: Reference source not found ataanguka:
Yaani ufalme wa IranError: Reference source not found utakwisha na utawala wake utatokomea na utawala mpya utatokezea yaani katika mwaka 1978l79 ubashiri huu umetokezea kuwa kweli wakati Shah Muhammad Riza Pahlawi alipopinduliwa na umma wa Waislam chini ya uongozi shupavu wa marehemu Ayatullah Ruhullah Al–Musawi al– Khomeini (a. r.) utawala wa Shah ulidumu zaidi ya karne mbili na nusu.

(17). Amir wa MisriError: Reference source not found atauawa:

Atakuwa ni mtu mmoja mwenye mamlaka ya utawala na atakuwa ni mtu mashuhuri katika Misri. Error: Reference source not foundKatika Kiarabu hapa neno lililotumiwa ni Amir yaani hakukutumiwa jina la Sultani au Malkia hivyo inatudhihirishia aina ya utawala utakaokuwepo wakati huo.

(18). Kuteketezwa kwa SyriaError: Reference source not found :
Kutakuwa na benderaError: Reference source not found zilizoinuliwa kutokea MisriError: Reference source not found zikielekea SyriaError: Reference source not found na kutatokezea bendera moja kutokezea Khorasan na bendera zote hizi tatu zitadai kumiliki Syria na wote hawa watapigania katika ardhi ya Syria. Vita ambavyo vitaangamiza na kuteketeza Syria.

(19). Majeshi kupitia mipaka ya Magharibi wataingia SyriaError: Reference source not found :
Yaani inawezekana majeshi ya Wazungu na nchi za Magharibi zitaingia SyriaError: Reference source not found kupitia Uturuki ili kuikalia Syria.

(20). Bendera rangi nyeusi
Bendera rangi nyeusi zitachomoza kutoka Khorasan (Labda linamaanisha jeshi la Hasan Sayyid).

(21). Kutajengwa njia za kupita chini ya ardhi kutokea mto wa Furati.
Kipitio hicho kitapitia KufaError: Reference source not found na itauletea utajiri mji huo. Wakazi wake watakuwa idadi kubwa na utashamiri (Ubashiri huu umeshatokea na kukamilika pia).

(22). Watu sitini
Kutatokezea watu sitini, watu wenyewe watakuwa waovu na majangiri ambao watadai kuwa wao ni mitume kwa hakika kutokana na wanavyovutia na wanavyojionyesha wataweza kuwavuta watu wengi upande wao (kiasi cha watu hamsini na nane wameishatokezea kudai utume hadi leo).

(23). Sayyid waongo kumi na wawili :
Kutokana na kizazi cha Abu Talib watu kumi na wawili watadai kuwa wao ni Imam, kizazi cha Imam au warithi wa Imam au wao ni MahdiError: Reference source not found (baadhi ya watu wameshatokezea na wameshapita na wengine bado watatokezea nao pia watapita).

(24). Mtu atachomwa motoError: Reference source not found
Mtu mwenye heshima sana kutoka Bani Abbas atachomwa motoError: Reference source not found hai baina ya Jehula na Khanqin (tunaweza kusema kuwa huyo mtu ni Abdus Salaam Arif ambaye aliungua moto katika ajali ya ndege)

(25). Kujengwa daraja mpya
Kujengwa daraja mpya katika mto wa Tigris katika upande wa Karkh, kutajengwa daraja huko BaghdadError: Reference source not found (daraja kama hili lilijengwa miaka michache iliyopita labda kunaweza kujengwa daraja lingine jipya).

(26). Kuteketezwa kwa BaghdadError: Reference source not found:

Watu wengi wa mji wa BaghdadError: Reference source not found watauawa kutokana na mitetemeko mingi ya ardhi na kutatokezea maafaError: Reference source not found na tufani nyeusi wakati wa mchana ambapo kutaleta matishio mbalimbali kwa wakazi wa Baghdad.

(27). BasraError: Reference source not found itazama.
BasraError: Reference source not found itazama katika maji kufuatia tufani kubwa ya mawimbi ya maji makubwa (Wasomaji wanashauriwa kusoma Nahjul Balaqgha kwa utabiri huu).

(28). Magonjwa sugu yataenea duniani
Kutakuja kuangamizwa na magonjwa sugu yataenea duniani kote na itaua watu kwa idadi kubwa sana.

(29). Makundi makubwa mno ya nzigeError: Reference source not found
Kutakuwa na makundi makubwa mno ya nzigeError: Reference source not found duniani kote, vita vya wenyewe kwa wenyewe huko IraqError: Reference source not found, kutakuwa na umwagaji wa damuError: Reference source not found kupindukia duniani kote na kutokezea vita vikali sana huko IranError: Reference source not found baina ya makundi mawili kiasi cha watu elfu themanini watauawa (Au imekamilika mwaka 1978 l79) .

(30). Nyuso za wanadamu zitabadilika
Hali ya nyuso za wanadamu zitabadilika na zitageuka kuwa za nyani na nguruwe.

(31). Kutatokezea mkono karibu na jua
Kutatokezea mkono karibu na jua ambapo wakazi wa duniani wataona pamoja na kustaajabika (jambo hili litatokezea muda mchache kabla ya kudhihiri kwa MahdiError: Reference source not found a.s.).

(32). Kunyesha mvuaError: Reference source not found yenye fujo
Duniani kote kutaanza kunyesha mvuaError: Reference source not found yenye fujo sana kuanzia tarehe 16 Jamadi us-Thani hadi tarehe 10 Rajab.

Kila Mwislamu mwenye kuwa na imani kamili juu ya Allah swt anaamini kuwa mvua hainyeshi kwa sababu ya misimu tu bali ni kwa sababu za amri na idhini za Allah swt.

Allah swt anatuambia katika Quran Tukufu kuhusu mvua:
Sura 25, Furqan Aya 48
Naye ndiye azitumaye pepo kuwa bashara njema kabla ya rehema
yake ya mvua; na tunayateremsha kutoka mawinguni maji safi.

Sura 35,Fatir Aya 9:
Allah ndiye aliyetuma hewa inayopeleka mawingu.

Sura 6,An-Am Aya 6:
Sisi tumeifanya mbingu kuwa yenye kunyesha mvua iendeleayo.

Sura 15 Al-Hijr Aya 22:
Sisi tumefanya mawingu na kunyesha mvua kutoka mbinguni.

Sura 29 Ankabut,Aya 63:
Na ukiwauliza,'Ni nani ateremshaye maji na kuhuisha ardhi baada ya kufa kwake?' Bila shaka watasema 'Allah' .

Sura 50 Qaf Aya 9:
Na tumeyateremsha kutoka mawinguni maji yaliyobarikiwa, na kwa hayo tukaotesha mabustani na nafaka zivunwazo.

Sura 8 Anfal, Aya 11:
Na anakuteremshieni mani kutoka mawinguni ili kukutakasisheni.

Sura 40 Muminun, Aya 18:
Na tumeteremsha kutoka mawinguni maji kwa kiasi.

Katika Aya hizo Tukufu za Quran kuwa upepo ndio unaosafirisha mawingu kuelekea mashariki, magharibi au kaskazini na kusini. Yaani inachukua kwa amri za Allah swt. Vile vile tumeona waziwazi kuwa kunyesha kwa mvua na kiasi chake kinahusishwa na Allah swt.

Baada ya kusoma hizo Aya tukufu tumeona kuwa mvua imekuwa daima ni rehema na idhini ya Allah swt ndipo inaponyesha juu ya ardhi.

Imeonekana kuwa katika baadhi ya nyakati neema na baraka hii inakuwa imezuiliwa. Na katika sura hii kuna riwaya nyingi kutoka kwa Mtume Mtukufu s.a.w.w na Maimamu a.s. zinazotuambia tusali sala za Istisqaa.

Tunapata mapokezi kutoka vitabuni kuwa katika zama za Imam Ali a.s. na Maimamu a.s. wamekuwa wakIssali sala za Istisqaa kwa ajili ya kuomba mvua,na mvua zilikuwa zikinyesha.

Mvua hii isiyo na mpangilio itanyesha kabla ya kudhihiri kwa Imam Mahdi Error: Reference source not found a.s. na haijulikani kama itanyesha Mashariki ya Kati tu au mahala penginepo.

(33). Watu waliokufa watakuwa hai
Watu waliokufa watakuwa hai (matukio haya yatatokea muda mchache kabla ya kudhihiri kwa Imam Mahdi a.s. Baadhi ya vitabu vinataja majina ya watu wataofufuka kupata maisha mara ya pili).

(34). MisikitiError: Reference source not found itarembeshwa
MisikitiError: Reference source not found itarembeshwa kwa mabati ya dhahabu vile vile QuranError: Reference source not found tukufu itarembeshwa kwa nyuzi za dhahabu.

(35). Sehemu tatu duniani zitadidimia

Sehemu tatu duniani zitadidimia ardhini au zitamezwa na ardhi pamoja na wakazi wake,y a kwanza itakuwa katika upande wa Magharibi baadaye katika Mashariki na hatimaye katika Bara la Arabia

(36). Dini ya Islam itakuwa dhaifu.
Islamu itabakia kwa jina tu. Maamrisho ya dini yatapotea. Watu wataingiliana sana kiasi kwamba itakuwa vigumu sana kumwelewa Mwislamu na yule asiye Mwislamu yaani Waislamu watakuwa wamepoteza hata ile sura yao ya Kiislamu.

(37). Kufr itakithiri katika Islam:
Nchi za Kiislamu zitaiga mitindo na maisha ya nchi zile zisizo za Kiislam. Waislamu wataomba misaada kutoka wale wasio Waislamu. Nchi za Kiislamu watauana miongoni mwao, watagombana kwa kutaka urafiki wa nchi zile ambazo zinamkanushaAllah swt (nchi za Kiislamu zitagombana miongoni mwao kwa kushawishiwa na nchi zile zisizo za Kiislamu)7

(38). Utawala wa Bani Hashim:
Imam Ali a.s. amebashiri kuwa utawala wa Bani Hashim utakwisha duniani. Mtawala wa mwisho atakuwa kijana mmoja mdhaifu, asiye na ujuzi wala utaalamu wowote na vile vile atakuwa akifuata ushauri wa watu wengi (katika dunia hii leo kuna utawala wa Bani Hashim nchi moja tu duniani kote nayo ni Jordan).

(39). Miaka thelathini ya mwisho
Miaka thelathini ya mwisho katika karne atakayodhihiri Imam MahdiError: Reference source not found a.s. kutakuwa na vitu vya ajabu ajabu na vya kustaajabisha mno.

Tanbihi Kuanzia mwaka 1370 A. H. inahitaji uchambuzi hadi siku ya leo, dunia imeona maajabu ya mageuzi ya mapinduzi na mauaji ya kushtusha na mambo mengi ya ajabu ajabu yasiyoweza kusadikiwa na watu kuwa binadamu anaweza kufanya mambo haya maovu kwa binadamu mwenzake.

(41). Kufika kwa WaturukiError: Reference source not found
Kufika kwa WaturukiError: Reference source not found katika pembe la Bara la Arabia katika Hadith maneno ya Turki na Jazira yametumika. Wataalam wa uchambuzi wa maswala haya wanasema: “Neno Turuki linamaanisha WarusiError: Reference source not found na Jazira ni Bara la Arabia, hivyo ni ubashiri mmoja muhimu sana wa kuzingatia kuwa Warusi wataingia Bara la Arabia yaani inawezekana wakaingia kwa mabavu (kwa nguvu) au wanaweza kuingia kwa upole kwa kutumia njia nyinginezo (tunaona Warusi wameingia katika Bara la Arabia).

(42). WazunguError: Reference source not found kuingia katika PalestinaError: Reference source not found:
Watu wa Roma ni wazungu na Ramla ni PalestinaError: Reference source not found hivyo kutakuwa na mvutano wa hali ya juu katika Bara la Arabia kwa sababu ya kugombania nguvu baina ya Waamerika, WazunguError: Reference source not found na WarusiError: Reference source not found.

(43). Mtu mwenye kuheshimiwa
Mtu mwenye kuheshimiwa mno kutoka Bani Abbas atatoswa majini katika mto Tigiris karibu na daraja jipya huko BaghdadError: Reference source not found.

(44). Kijiji cha Jabiya
Kijiji cha Jabiya karibu na Damascus itadidimia ardhini.

(45). Ziwa Sawa
Ziwa Sawa litajaa kwa maji kwa mara nyingine tena. Ziwa hili liko karibu na mji mtukufu wa Qum lilikauka pale Mtume s. a. w. w alipozaliwa. Wale wote wanaokwenda ziara ya Masuma –i–Qum wanashuhudia ubashiri huu.

(46). Wanawake na watoto
Watoto na wanawake watakuwa watawala.

(47). Taratibu za tawala za nchi
Taratibu za tawala za nchi zitakuwa zikipata sura mpya mpya za kutawala vile vile utawala wa kifalme utatokomea.

(48). Kizingiti baina ya ardhi na mbingu
Kutaonekana kitu kama kizingiti baina ya ardhi na mbingu, kweli litakuwa ni jambo la kustaajabisha kabisa hasa Mashariki ya Kati.

(49). Jumuiya ya wale wasio waumini
Jumuiya ya wale wasio waumini wataenea Bara la Arabia na nchi nyingine za Kiarabu (ama wao ni WarusiError: Reference source not found au WachinaError: Reference source not found kwani Warusi wameishajidhatiti katika nchi nyingi za Kiarabu).

(50). Kuwasili kwa WachinaError: Reference source not found
Kuwasili kwa WachinaError: Reference source not found katika Bara la Arabia ni ubashiri mkubwa wa vita vikubwa hali mbaya kabisa isiyoelezeka itatokea baada ya wao kuwasili huko.

(51). Michafuko ya kila aina
Kutakuwa na michafuko ya aina mbalimbali kuanzia Azarbaijan na Armenia. Machafuko haya yataenea hadi mlima mwekundu. Matokeo haya na hatima yake yatakuwa mabaya kiasi kwamba watoto watakuwa kama wamezeeka na wazee watatamani mauti. Machafuko haya yatafika mpaka mji wa KufaError: Reference source not found kupitia Wast na vita hatari kabisa vitatokea karibu na mji wa Najaf. Kwa hakika maovu na matisho haya hayaelezeki. Vile vile vita vitatokezea karibu na Teheran.

(52). Kuzuia kizazi
Kutakuwa na mipango mbalimbali ya kuzuia kizazi na mbinu hizo zitashurutishwa kwa njia mbalimbali.

1. Habari hizi tazama Day of Judgement ,Sayyid Saeed Akhtar Rizvi,Bilal Muslim Mission of Tanzani,DSM,chapa ya pili,1978,uk. 44. ,naye amenakili kutoka Bihar-ul- Anwar,j. III.

2. Kwa msomaji atakayependa kufanya utafiti zaidi juu ya swala hili juu ya Ubashiri,anaweza kusoma Hotuba ya Imam Ali a.s. Al-Makhzun katika kitabu kiitwacho Basharatul-Islam,chapa ya Baghdad.

3. Leo duniani tunaona kuwa maendeleo ya sayansi yametudhihirishia kuwa kuna uwezekano wa kufikisha Sauti na sura duniani kote hasa kwa kupitia satellites. Sasa jee kuna ugumu gani kwake Allah swt kufanya kudra zake?

4. Mambo kama haya ndivyo yanavyotokea katika kupiga kura za kidemokrasia!

5. Kwa utumwa hapa kunamaanisha mbinu za kumfanya mtu asiweze kusema dhidi ya mambo ya mfadhili wake kama vile tunavyoona na kusikia kuhusu masharti ya misaada itolewayo na nchi na watu wafadhili.

6. Nimesikia katika Idhaa ya Kiswahili ya BBC mnamo tarehe 17 Novemba 1995 saa 6. 30 jioni kuwa Chuo Kikuu cha Al-Azhar University cha huko Misri kimetoa fatwa kuwa mwanamme anaweza kujigeuza k,uwa mwanamke na vile vile mwanamke anaweza kugeuzwa kuwa mwanamme kwa njia za operesheni ati kwa sababu ni maumbile yake ndivyo yalivyo.

Vile vile nimesikia katika idhaa ya Kiingereza ya BBC hivi majuzi (wiki moja kabla ya Fatwa kutoka Al-Azhar) kuwa kumefanywa uchunguzi na utafiti huko Amerika na kutolewa ripoti kuwa mtu khanisi na anayelawiti na kulawitiwa aachwe awe hivyo na wala asilaumiwe na jamii kwa sababu ndivyo yalivyo maumbile yake.

7. Tunajionea vile nchi za Kiarabu zinavyopingana na kupigana wenyewe kwa wenyewe kwa ajili ya ushawishi wa nchi za Magharibi. Utengano miongoni mwao unatokana na kulaghaiwa na nchi za Magharibi ambavyo ni vyema kwa maslahi yao.

Source URL: https://www.al-islam.org/node/24307